# LEARNING BY EAR

## "WAGENI VIZABIZABINA MSOALIKWA- VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA UGONJWA WA MALARIA"

## KIPINDI CHA TISA: "UMOJA NI NGUVU"

**SCRIPT: CHRISPIN MWAKIDEU**

**EDITOR: ANDREA SCHMIDT**

**ASSISTANT EDITOR: KATRIN OGUNSADE**

**HEALTH EXPERT: DR. HEIDRUN HÜBNER**

**List of characters for episode 9:**

- MASIKA (40)
- BETTINA (34)
- KAREMBO (14)
- ZAWADI(BABY, no actor)
- MAMA DAVID (43)
- DAVID (14)
- HEADTEACHER(38, female)

**INTRO/NARRATOR (same voice):**
Nawasalimu tena na karibuni katika noa bongo Jenga maisha yako kwenye mchezo wa kuigiza **" WAGENI KIZABIZABINA MSOALIKWA-VITA VYA FAMILIA MOJA DHIDI YA MALARIA"** Wiki iliyopita tulimuacha david akienda kumueleza mamake kuhusu mpango wake na Karembo wa kuanzisha chama cha kupambana na malaria na karembo akatangaza hali ya hatari dhidi ya mbu na kuapa kwamba atavifyeka vichaka vyote,na kuyaondoa maji yaliotuwa na kuamirisha mayai yote ya mbu. Masika, babake karembo, alijiunga na vita hivyo kwa kuzinduwa upya vidimbwi vilivyokuwa vikikuziwa samaki.na hii ilimuacha Betina bila mchango wake. Je, karembo atafaulu? Jiunge nasi katika sehemu hii ya tisa ya kisa **"UMOJA NI NGUVU".**

**MUSIC INTERLUDE**

**<u>SCENE ONE: EVENING AT MAMA DAVID'S HOUSE.</u>**

**A-SFX: BOILING OR FRYING OF SOME FOOD**

1. **DAVID:** Mama..
(**POLITELY)**
Nikusaidie na chochote?

2. **MAMA DAVID:** (**STUNNED)**
Hmm..maajabu ya musa..yaani leo wataka kunisaidia?

3. **DAVID:** Ndio... najuwa ilivyokuwa tabu kunilea mimi ukiwa mjane... .. na
mara nyingi nimekuaibisha lakini mimi hukufurahia kama mamangu.

| | | |
|---|---|---|
| **4.** | **MAMA DAVID:** | Mmmh... leo umesema maneno mazuri sana mwanangu..... shule ilikuwaje? Na karembo anaendeleaje? Unajuwa bado wazazi wake wananilaumu kwa ugonjwa wake ilhali mimi nilikuwa nataka kumsaidia apone.... |
| **5.** | **DAVID:** | Shuleni ni kuzuri... leo tulitembelewa na dkt Munga kutoka hospitali ya wilaya ya Ribo.. ambaye alituzungumzia kuhusu malaria. Tulijifunza mambo mengi, kumbe hizi dawa wanazouza vibandani ili kutibu malaria hazifai tena kwani vimelea vya malaria vimezizidi nguvu? |
| **6.** | **MAMA DAVID:** | Ndio maana mimi ninaamini dawa za kienyeji.miti ni dawa..hata hivyo,endelea mwanangu. |
| **7.** | **DAVID:** | **(CAUTIOUSLY)**<br>Karembo alirudi shuleni leo,amepona kabisa na ni mzima wa afya..anataka kuanzisha chama cha kupambana na malaria,mama waonaje nijiunge naye? |

**(SHORT SILENCE)**

| | | |
|---|---|---|
| **8.** | **MAMA DAVID:** | (**TAKES ONE DEEP BREATH)**<br>Hebu njoo karibu,fungua hili dirisha,najua ni usiku na kuna giza lakini lifungue tu.. |

**9. B-SFX: WINDOW SLOWLY OPENING. CRICKETS SOUNDS**

| | | |
|---|---|---|
| **10.** | **MAMA DAVID:** | Unaona nini nje? |

| | | |
|---|---|---|
| 11. | **DAVID:** | Kiza..naona kiza tu,mama kwani kuna nini,u mzima kweli? |
| 12. | **MAMA DAVID:** | Sina neno!,kuamini madawa ya kienyeji hakuna maana kuwa mimi ni kichaa,haya basi niambie nyuma ya nyumba yetu kuna nini? |
| 13. | **DAVID:** | Nyuma ya nyumba?,hamna chochote,isipokua nyasi za mzumai unazopenda kupikia chai. |
| 14. | **MAMA DAVID:** | Aha! Lakini ulijuwa kuwa huo mmea pia unaitwa" mnyasi wa homa" na pia harufu yake hufukuza mbu... nilijifunza yote haya kutoka kwa mizanja |
| 15. | **DAVID:** | **(SURPRISED)**<br>Ati nini?sina habari.... kwa hivyo ndio sababu ulinishurutisha nisiwashe dawa ya mbu? Kwa sababu ulitumia mzumai? Sasa nimeelewa.. mama wewe ni mjanja!! |
| 16. | **. MAMA DAVID:** | Nashukuru mwanangu kwamba wewe na karembo munataka kuanza huo mwito na mimi nitawapa msaada wowote munaotaka. |
| 17. | **DAVID:** | Siamini!<br>**(NOT BELIEVING)**<br>Unamaanisha uyasemayo mama? |

**18. MAMA DAVID:** Bila shaka!,sasa hebu funga hilo dirisha kisha uketi mezani upate kula cha jioni.

**19. C-SFX: WINDOW CLOSES**

**NARRATOR:** David alikuwa bado haamini aliyojifunza na siku iliyofuata hakuweza kungoja ili kumueleza karembo..kwa hiyo kengele ya mapumziko ilipolia tu..

**<u>SCENE TWO: BREAK TIME AT KAREMBO'S SCHOOL</u>**

**20. D-SFX: SCHOOL BELL RINGS...FOLLOWED BY BURST OF NOISE FROM STUDENTS.**

**21. DAVID:** **(EXCITED)**
Karembo, hutaamini masikio yako!

**22. KAREMBO:** Hebu makinika David kwani umeona jinamizi nini?uliongea na mamako?

**23. DAVID:** **(IN TRANCE)**
Ulijua kuhusu mzumai?

**24. KAREMBO:** Ni nani asiyeujuwa si unatumiwa kwa chai?

**25. DAVID:** Hatimaye najua jambo usilolijua..basi mmea huo hautumiki tu kwa chai bali ni mzuri kwa kufukuza wageni wasoalikwa..unaamini hayo?

**26. KAREMBO:** La.ulijifunzia wapi hayo?

**27. DAVID:** **(HESITANT)**
Tuseme aliyenifunza ni mtu ambaye ninamuamini mamangu pia ali...

**28. KAREMBO:** (**CUTS HIM SHORT)**
Nilijuwa hatakubali ujiunge na chama chetu... lakini si neno nimeweka vibandiko hapa shuleni kwa mwanafunzi yeyote anayetaka kujiunga na tayari wengi wameandika majina yao

**29. DAVID:** La, nilitaka kukuarifu kuwa mamangu mbali na kuniruhusu nijiunge na chama chako pia amesema atatupa msaada wowote tunaotaka...

**30. KAREMBO:** Nafurahi kusikia hivyo.!.. sasa basi ni muhimu.

**31. E-SFX: SCHOOL BELL RINGS, FOLLOWED BY NOISY STUDENTS**

**32. H/TEACHER:** Karembo! David! Hebu Njooni ofisini mwangu haraka!

**33. DAVID:** **(TERRIFIED)**
Karembo kwani tumekosea nini?mimi naogopa kuadhibiwa..

**34. KAREMBO:** David, mimi ndio ninaefaa kuogopa,wewe ni mvulana.acha hofu sidhani kuna mabaya tulotenda.

**35. F-SFX: DOOR BEING KNOCKED.**

| | | |
|---|---|---|
| **36.** | **H/TEACHER:** | Ingieni!<br>**(STERNLY)**<br>ni nani aliyetundika ile ilani katika ubao wa mawasiliano? Na kwa ruhusa ya nani? |
| **37.** | **DAVID:** | Si mimi mwalimu..ni.. |
| **38.** | **KAREMBO:** | Ni mimi. Baada ya kuuguwa niliona nifanye kitu kuhusu malaria.. lakini kama nimekosa basi nitazitoa ilani hizo ninaporudi darasani. |
| **39.** | **H/TEACHER:** | Kwanini?kwanini uzitoe sasa baada ya kuziweka?<br>(**PAUSE)**<br>Hilo ni wazo zuri ajabu ! sijui kwanini hatukufikiria kuanzisha chama kama hicho miaka yote hii? |
| **40.** | **KAREMBO:** | **(RELIEVED)**<br>Kwa hivyo hukukasirishwa na nilivyofanya? |
| **41.** | **H/TEACHER:** | Njia uliyotumia ndio haikuridhisha.. lakini kwa vile litawafaidi wanafunzi wengi nimeamua kuwa shule nzima itajiunga na chama hicho. |
| **42.** | **KAREMBO/DAVID:** | **(HUGE SURPRISE)**<br>Shule yote? |
| **43.** | **H/TEACHER:** | Ndio, nitawaomba hata waalimu na wafanyakazi wote wajiunge. wahenga walisema kidole kimoja hakivunji chawa. Sasa nataka uanze kufikiria |

malengo yako na jinsi ya kuongoza? Nitazungumza na wizara ya afya kwa niaba yako iwapo utahitaji msaada wowote.

**44. KAREMBO:** **(IN DISBELIEF)**
Mimi..sikujua kuwa itakua kazi kubwa hivi..nina wasiwasi sasa..

**45. H/TEACHER:** usiwe na hofu... tutaungana pamoja... ni hayo tu kwa sasa. nifungieni mlango munaporudi darasani.

**46. G-SFX: DOOR SLOWLY CLOSES.**

**NARRATOR:** na hivyo ndivyo ilivyokuwa... shule yote ya karembo ikajiunga katika kupiga vita malaria.. karembo akawagawanya makundi makundi, na kampeni ikaanza, lengo lao kuu likiwa kuwaangamiza mbu au kama alivyopenda kuwaita karembo... wageni wasoalikwa! Je, nyumbani kwa masika kuna yapi?

**SCENE THREE: AT MASIKA'S HOME**

**47. H-SFX (RADIO PLAYING LOUD LOCAL MUSIC AS MASIKA LISTENS)**

**48. BETTINA:** Masika, nahitaji kuzungumza na wewe

**49. MASIKA:** **(NOT HEARING)**
Unazungumza na mimi?

**50. BETTINA:** Hapana! Nasema na ukuta! Ikiwa sisemi na wewe itakuwa nasema na nani? Hapa muko wewe na zawadi .. Hebu punguza hiyo redio...

**51. I-SFX (RADIO VOLUME LOWERED BUT PLAYS IN BACKGROUND)**

**52. BETTINA:** Mbona mwanitenga? Hizi harakati za malaria.. kila mtu anawajibika isipokuwa mimi tu, wewe unaendelea vyema na mambo ya samaki... karembo amefanya kazi chungunzima kuhusu mazingira ya hapa nyumbani na amenieleza ameanza chama shuleni kwao cha kupambana na malaria, sasa mimi itakuwa ni jikoni tu?

**53. MASIKA:** Mchango wako mkubwa ni kunilelea wanangu, uhakikishe wamekua bila sinyesinye yeyote kwa kila hali! Mengine niwachie mimi..

**54. BETTINA:** Kwanini? Kwanini nisishughulike? Hata mimi nataka kuwa katika harakati hizi na najuwa naweza kufanya jambo la msingi!

**55. MASIKA:** **(WITH EXCITEMENT)**
nimekumbuka kitu... kwanini basi usiende kwa mamake david ukamtake radhi kwa niaba yetu? unajuwa sikupenda kwake hata yeye alitaka kutusaidia.

**56. BETTINA:** **(REGRETFULLY)**
Kweli!hata nilikuwa nimesahau kumuhusu...

alitusaidia sana wakati wa uja-uzito wangu...na itakuwa si sawa kwa jambo moja kutuvunjia usuhuba wetu. Masika hebu nipe samaki kidogo nikampe kama kumradhi yetu... naenda kwake sasa hivi...

**57. MASIKA:** Ala!sasa na Zawadi je?

**58. BETTINA:** Akilala humo chini ya neti huwa hana usingizi wa man'gamun'gamu... hulala kama pono... tena kwa muda mrefu... bora usipandishe sauti ya redio itamuamsha...

**NARRATOR:** Akifuliza na samaki mkononi, betina alielekea kwa mamake david.aliona haya na aibu na kujuta ndani yanafsi yake lakini hakujali.je, mamake david atakubali kuwasamehe? Tega sikio kwa yatakayosibu...

**SCENE FOUR: BETTINA AT MAMA DAVID'S HOUSE.**

**59. J-SFX: CEREAL BEING POUNDED**

**60. BETTINA:** Hodi huku... mamake david,. (**BIT UNSURE)** nakuona unatwanga mahindi.. nikusaidie?

**61. MAMA DAVID:** **(BREATHING HEAVILY)**
Umekuja kutafuta nini hapa kwangu betina baada ya kuniita mchawi wa kijiji hiki?

**62. BETTINA:** La! Sijawahi hata siku moja kusema hivyo.. niko hapa kukutaka radhi kwa niaba yangu na

mumewangu... tulikosea siku ile tuliyogombana... na huyu hapa ni samaki ametoka kwetu..

**63. K-SFX: SOMETHING BEING UNWRAPPED**

**64. MAMA DAVID:** Yaani hivi vijisamaki viwili tu ndio vyakunihonga mimi nisahau madhila yote yale? Eh?
**(STARTS TO LAUGH)**
usiniambie umeogopa! Betina, tumekuwa marafiki kwa siku nyingi... hatuwezi kuekeana chuki daima.. haya nisaidie kutwangwa. Nilikusamehe kitambo..

**(BOTH LAUGH OUT)**

**65. BETTINA:** Asante sana... nashukuru kwa kuukubali msamaha wetu .. nataka ushauri... unajuwa uvumbuzi wa masika katika kuangamiza mbu na karembo alivyoanzisha chama cha kupinga malaria shuleni kwao. Pia mimi nataka nianze mradi fulani lakini nimepungukiwa na mawazo... nifanye nini?

**66. MAMA DAVID:** (**THOUGHTFULLY)**
Kwanini usirudi kwa mizanja, unajuwa yeye anajuwa mengi..

**67. BETTINA:** **( VERY ANNOYED)**
Ati nini? Umeniambia nini? Mizanja? Utanituma vipi tena kwa yule mganga na unajuwa yaliotokea tulipoenda na karembo?

**68. MAMA DAVID:** **(ALSO ANNOYED NOW)**
Usinilaumu kwa yaliyotokea!wewe ndiye uliyetaka usaidizi na ushauri kutoka kwangu.ala!

**69. BETTINA:** Kumbe nilipoteza muda wangu kuja hapa... wewe ni yule yule! Hujabadilika! Na hautabadilika kamwe!!

**70. MAMA DAVID:** Wala sina haja ya kubadilika,haya chukua hilo vumba lako la samaki na uione paa nyumba yangu!!

**71. (AS THE ARGUEMENT SOARS, KAREMBO AND DAVID ENTER)**

**72. KAREMBO/DAVID:** **(SURPRISED)**
Mama!!

**OUTRI/NARRATOR:** Ilikuwa ni sehemu ya Tisa ya mchezo wageni vizabizabina wasoalikwa,vita vya familia dhidi ya Malaria.Karembo na David wameshangazwa na mzozo mkali kati ya mama zao... kweli uswahiba wao umevunjika? Na je tutaona mabadiliko yeyote kuhusu kuangamiza mbu na malaria baada ya bidii ya masika , karembo na wengineo? Usikose kujiunga nasi katika sehemu ya kumi nay a mwisho ya mchezo huo wa kuigiza kutoka DW.Ukitaka kusikilza tena mchezo huo au kutupa maoni yako tembelea tovuti yetu www.dw-world.de/lbe

Hadi wakati mwengine..kwaheri.